**TEGA SIKIO UJIFUNZE: EPISODE 7**

**<u>"KWANINI WATU HUOTA'</u>**

Mchezo umeandikwa na Lydia Heller

Mwelekezi : Maja Dreyer

Tafsiri: Eric Ponda

**<u>WAHUSIKA</u>**

| | |
|---|---|
| Mtangazaji | |
| Jenny | (14) |
| Jack | (15) |
| Nyanyake Jack | Kikongwe |
| Mfalme muigizaji | Sauti ya hadhi |

**<u>SEHEMU</u>**

Nyumbani kwa Jack

Nje (chini ya Mti)

**<u>Sauti</u>**

Muziki wa filamu chini kwa chini Celine Dion au out of 10,000 BC

Muziki wacheza kisha kukatika ghfla (Jack afunga filamu)

Mchakacho wa viazi Chips kwenye mfuko.

Akiondoa glasi

Sahani zikigongana

Mchakacho wa mifuko ya alumini

Hatua zikikaribia

Wadudu wakivuma

Ndege wakimba

Pumzi nyepesi Mtu akikoroma

---

INTRO:
(Mtangazaji

Hujambo na karibu tena Mfululizo wa makala yetu ya mchezo wa kuigiza makala ya "Tega Sikio Ujifunze". Kujifunza kwa Kusikiliza 'Ufahamu wa Mambo ya Kila Siku'. Hata hivyo safari hii hatuzungumzii mambo hasa ya kila siku bali ni zaidi kuhusu usiku na kulala. Hasa, tunazungumzia ndoto tunazopata wakati tukiwa usingizini. Mjadala wenyewe unaanza kimapenzi---Jack anamualika Jenny watazame pamoja filamu na wakati mambo yalipokuwa yanaemdelea vyema na ndoto zake kukaribia kutekelezwa, Jenny anajitokeza na yale maswali yake ya kawaida, ambalo hata halikaribiani na swala la mapenzi. Anauliza 'Kwa nini watu huwa wanaota ndoto'

---

1. Scene

---

*( muziki wa sinema wasikika chini kwa chini, sauti ya mfuko wa plastiki wa viazi/ mikono ikiingia kwenye mfuko huo/ viazi vikitafunwa)*

**Jack:** *(akinong'ona, nahuku akiamuru)* Nyamaza Jenny! Wacha kuleta rabsha! (*anapumua kwa nguvu)* Sasa! Sikiliza kwa makini, huyu mfalme mzee anakaribia kusema matamshi muhimu zaidi katika filamu hii'

**Mcheza filamu:(**Mwanamume)
Na mwishowe nyinyi wapenzi wawili mnakuwa viongozi wa nchi hii ya milima manjano *(muziki kidogo halafu anaendelea)* Kwa sababu nyinyi daima mumekuwa mukiamini ndoto zenu zitatimia.' (*Punguza muziki mara nyingine)*

**Jenny:** *(akizungumza huku filamu ikiendelea) (akiwa na hasira)* Hii si filamu nzuri *(anakula kiazi)* Bado inaendelea?'

*Muziki wa filamu unacheza halafu unakwama ghafla (Jack anaizima filamu)*

Jack: *(akipumua kwa nguvu, halafu kwa hasira)* 'Hapana haiendelei.....imemalizika. Sitawahi kutazama filamu na wewe tena! Wewe ni kulalamika tu.. hutulii!. Ingawa ni filamu poa sana. Kuna mtu na mkewe wanabishana halafu wanapatana wakiamini ndoto zao, na kadhalika..'.

**Jenny:** *( akiwa ameudhika)*' Unamaana kuwa hii ni filamu poa? Wewe ndiye uliyekuwa ukilia sasa hivi.'

**Jack:** *( kwa dhati)*' Sikuwa nikilia'

**Jenny:** *(akimtania)*'Kwa hiyo hukutoa hata tone moja la machozi? Kuna machozi yalikuwa yakitoka machoni mwako kisha baada ya kuyafuta machozi hayo kitu

kingine kilikuingia puani.'

**Jack:** *(kwa unyonge)*'Kwa kweli nilifikiria ni poa kwamba wote wawili waliungana na kusimama pamoja katika hiyo filamu-- Haijalishi kilichotokea au kusemwa, muhimu ni kwamba walisimama kidete na kutiana imani kuhakikisha kwamba ndoto zao zinatimia! Kwa nini unacheka? Kuna ubaya gani kwani?'

**Jenny:** *(akitabasamu)* 'Nilikuwa nafikiria kile ambacho kingetokea ikiwa ndoto zangu zingetimia. Nitashikwa na wazimu! Sijui kwanini mimi hufikiria mambo yasiyokuwa na maana.'

**Jack:** *(akibishana)* 'Si ndoto aina hiyo lakini!'

**Jenny:** 'Najua, najua, lakini kwa kweli sielewi ni kwa nini tunasema hivyo. Kwa mfamo tunasema naota kuwa mchezaji kandanda au ikiwa nitapunguza kilo tatu katika uzito wangu si nitakuwa na umbo lile ninalo-ota....!'

**Jack:** *(anamkatiza, huku akimchezea)* 'Kilo tatu hazitoshi.'

**Jenny:** 'Aah nyamaza wewe! Ninamaanisha inaonekana kana kwamba ndoto ni sawa na matarajio.'

**Jack:** 'Au mawazo au malengo.'

**Jenny:** 'Hasa! Lakini huo ni upuuzi mtupu. Daima nimetamani kuwa mchezaji kandanda hodari wa kulipwa, lakini sijawahi kuwa na ndoto hiyo... yaani nikiwa usingizini! Wakati mwengine huota ni kuruka na wakati mwengine kuukimbilia mpira, lakini najipata kukwama mahali pamoja. Jambo la aina hiyo *(anacheka)* linanizuia kuwa mcheza kandanda wa kulipwa ikiwa ingebainika. Yaani namaanisha kuwa ndoto hazina maana.! Mimi hujiuliza ndoto zina maana gani na kwa nini tunaota?'

---

**MUZIKI…..**

---

2. Scene

*Bilauri zinawekwa/ sahani zagongana/ mifuko ya plastiki yatoa sauti/ hatua za miguu (Jack anasafisha)*

**Jack:** *(akiwa na hasira huku akimuiga Jenny)* 'Lakini kwa nini huwa tunaota? *(Akisema kimoyomoyo)* Jenny ni mm..shamba. *(akichakura chakura)*Sasa

nimekwama kama mpumbavu. Lakini naapa sita... *(akishtuka)* NYANYA???

**Nyanyake Jack:** *(akiwa na wasi wasi)*'Aah pole mjukuu wangu! Sikutaka kukushtua. Nilisikia mtu akiongea chumbani na nikataka kujua kinachoendelea. Unaondoa vyombo? Kwani Jenny ameshaondoka?'

**Jack:** *(akiwa amaudhika)* 'Hapana'

**Nyanya:** 'Kwani mumebishana'

**Jack:** *(kwa hasira huku akichakurachakura)* 'Nyanya hayakuhusu haya! *(anapumua)* Sawa, sawa. Hebu nieleze. Ni kweli kwamba ndoto hazina maana?

**Nyanya***:(kwa imani)* 'Hapana hata kidogo. Kwani Jenny alisema hivyo? Kwani Jenny yuko macho sana? Au ni mtu wa mambo mengi?

**Jack:** *(akiwa amechanganyikiwa)* 'Mambo mengi? Yawezekana. Sasa nyanya niziweke wapi hizi njugu?'

Nyanya: 'Ziweke hapo juu ya kabati'

*(Anaweka sahani kwenye mbao)*

**Jack:** 'Lakini hiyo inahusiano gani na kuota?'

**Nyanya:** Wakati mtu anapoota, akili huwa inafanya mambo kama vile ufanyavyo sasa.

**Jack:** *(akiwa amechanganyikiwa)*Kuongea na Nyanya!

**Nyanya:** Usiwe pumbavu nawe, akili huwa ikipanga mambo!

**Jack***:(akiwa bado amechanganyikiwa)* Kupanga mambo vipi?

**Nyanya:** 'Wakati tunapolala, akili huwa hailali, huwa inatafakari mambo yote iliyoshuhudia wakati ukiwa macho katika mpangilio fulani, inatenga yale muhimu na kuhifadhi yale mapya. Kama vile wewe unavyoendelea na kazi yako ya kusafisha. Unaweka sahani, unatupa maganda ya njugu, na kadhalika... Wakati akili inapotaka kuhifadhi jambo mahali muafaka na kwa mfano kuchakura kwenye kabati, ili kutafuta mahali muafaka pa kuliweka, wakati mwengine huleta mawazoni mambo yaliyo sahaulika kitambo. Hizo ndizo ndoto.'

Jack: 'Kwa hivyo kuota ni kama kupangilia? Sasa naelewa.'

Nyanya: (*akifurahi kwamba ameweza kueleza hadi kueleweka)* 'Ni vyema. Na pia ndoto daima huwa za dakika chache tu. Na kwa kawaida tunaota ndoto punde tu kabla ya kuamka. Na wakati akili ikikamilisha kupanga panapohitajika, tunagutuka na kuamka.'

Jack: *(akicheka huku akiwa hamsikilizi tena nyanyake)*'Kwa hivyo Jenny anasema kweli....kuota ni kama kupangilia na hivyo si muhimu kabisa!'

---

MUZIKI

---

3. Scene:

---

*(Jenny yuko nje amelala chini ya mti) wadudu wanavuma huku na huko katika hali ya joto Ndege wanaimba......Kunasikika sauti ya kupumua kwa undani, na kukroma. Hatua za haraka zikikaribia..*

**Jack:** *( Anaitaka, kwanza kutoka mbali, halafu anakaribia)* 'Jenny! Je...nny *(akiongea pekee)* Ah yule pale, chini ya mti....Ni lazima awe ni yeye yule....'

(*Hatua mtu akitembea)*

**Jack:** *(anawasili, akihema haraka)* 'Jenny habari. Nataka kukwambia kitu. Kwa kweli hukukosea!'

**Jenny:** (*anavuta pumzi, huku akikoroma kidogo-kidogo)*

**Jack:** *(akiwa amechanganyikiwa)* 'Umelala, au vipi? *(Jenny aendelea kuvuta pumzi)* Wacha mzaha.eti amelala chini ya mti! *(anamsukasuka kidogo)* Nitafunga pua yake na labda atawacha kukoroma!'

Jenny: (*akivuta pumzi kwa nguvu)…*

**Jack:** *(akiwa na hofu sana)* 'Oh Mungu wangu, ni nini mbaya? Macho ya Jenny yanacheza-cheza! (akitaharuki) Labda amezirai! *(akiwa na wasi wasi)* Nifanyeje sasa Mungu wangu? *(aitana, akihofia)* Jenny, Jenny, amka tafadhali amka!'

**Jenny:** *(akiwa bado usingizini)* 'Kuna nini kwani? Fujo ya nini hii? Mbona umebadilika sura, nini mbaya?'

**Jack:** *(akifurahi)* 'Jenny!... ni bahati sana …Ungali hai?'

**Jenny:** *(haelewi kinachoendelea)* 'Nini?'

**Jack:** *(akiongea kamaishujaa)*'Jenny, una bahati kwamba nilikuwa nikipita karibu na hapa! Ulikuwa umelala chini ya mti, nikaja upande wako na nikakukuta kuwa umezirai huku macho yako yakipepesa-pepesa, na mimi sikufikiria na.......

**Jenny:** *(anamktaiza)* 'Jack? Pole kwa kukatiza hadithi yako lakimi si eti umeniokoa bali ni kunikatizia zoezi langu la usingizi la REM.'

**Jack:** *(hana raha)* Usingizi wa REM ni nini?'

**Jenny:** *(akimsomea)* 'REM inamaanisha macho kupepesa pesa kwa haraka, na watafiti wanaiita hali hiyo usingizi wa REM.

**Jack:** *(hajaelewa kitu)* 'Kwa hivyo?'

**Jenny:** 'Huo ndio wakati tunapoota....wakati huo wa usingizi wa macho kupepesa haraka.'

**Jack:** *(akiwa na hasira na akiongea ka sauti ya juu)*' Kwa hivyo inamaanisha kwamba nilikuwa na hofu na wasi wasi tu bure kuhusu maisha yako, ilhali wewe ulikuwa ukifanya zoezi la kuota? Hata hivyo umesema ndoto hazina maana?'

Jenny: *(kwa unyenyekevu)* 'Labda nilifanya haraka jana kutamka bila ya kufahamu tulipokuwa tukitazama ile filamu. Punde niliporejea nyumbani nilimuuliza mamangu kuhusu ndoto, na zina maana gani na kadhalika.. Daima yeye huwa anasoma zile kurasa za habari kuhusu familia katika magazeti na mara nyingi huwa zinaandikwa habari kama hizo. Hata hivyo alisema ndoto ni muhimu. Ni kama...

**Jack:** *(anamkatiza kwa kujionyesha anajua)* 'Ni kama kusafisha akili, sio?'

**Jenny:** *(akishangaa)* ' Wacha upuuzi! *(anasita kidogo, halafu anafikiria kwa kuongea)* 'Ikiwa ni kama kusafisha akili basi hazina maana *(anacheka)* Kwa kweli hayo ndiyo maoni yangu kuhusu kusafisha.'

**Jack:** 'Ahaa'

**Jenny:** *(akiendelea bila kusita)* 'Mamangu aliniambia kwamba watafiti hawaja kubaliana kuhusu maana na kazi ya ndoto, lakini wengi wanasema kuwa zina umuhimu wake. Wanasema mambo yote yanayo shuhudiwa wakati mtu akiwa macho huhifadhiwa katika sehemu ya ubongo kwa muda mfupi na hatimaye kuppelekwa katika ile sehemu ya kuhifadhiwa kwa muda mrefu. Kwa hiyo ina maanisha kwamba ndoto hufuta ile hifadhi ya muda mfupi. Mambo yasiyokuwa muhimu hutupwa baada ya kuyaona kwa kifupi katika ndoto zetu.'

Jack: *(kiubishi)* 'Si ni kama vile nilivyosema....ni kama kusafisha!'

**Jenny***:(akishtuka)* 'Ni kweli! Ni kama kusafisha *(anasita kwa muda halafu anaendelea)* Huo ndio ukweli tu kuhusu ndoto za jinamizi. Hata hivyo watafiti wengine wanasema kwamba ndoto ni kama kurudia mambo ambayo yalitugusa sana yalipotokea, kama vile ajali au mikosi ya kimaumbile.'

**Jack:** *( akiwa yashamtoka)* au kama kufagia vyumba vyetu.'

Jenny: *(akisomea)* 'Ndio, sawa kabisa. Na ndoto hutusaidia kupambanua mambo haya. Lakini watafiti wengine nao wanasema kuwa kuwa ndoto zaweza kutuonyesha jinsi ya kutatua matatizo sugu maishani tunapokuwa macho. Na wengine nao wanasema kuwa mdoto ni picha tu zinazokuja akilini bila mpangilio wowote. Au pengine ndoto huifanya akili kutolala ndipo tuweze kufanya shughuli zetu kama kawaida tunapoamka. Au....”

*(Pumzi zinavutwa kwa undani, na kukoroma hafifu)*

**Jenny:** ***(****anasita)* ' Jack?' *(kwa hasira)* Sasa analala*!(Jack anakoroma, Jenny ameshangazwa)* Wacha mzaha..... hii ni balaa Jack. Kuongea naye kuhusu ndoto ni kazi bure tu.'

---

MUZIKI

---

**OUTRO:**
(Mtangazaji)
Amkeni, amkeni. Asante kwa kuota pamoja nasi na kumbuka kwamba yeyote anayetaka kumwelimisha wake wa roho na habari hizi zote kuhusu usingizi na ndoto anawza kusikiliza kipindi hiki tena katika http://www.dw.de/kiswahili. Kipindi hiki ni ndoto ya Lydia Heller. Asante kwa kusikiliza. Kuwa masi tena wakati ujao. Kwaheri.